

# HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

## SHULE YA SEKONDARI TAMBARARE

S. L. P 278, HAI.

SIMU: 0758-920245

TAREHE: \_\_\_\_\_

Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi

---

---

YAH: MAELEZO YA AWALI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TAMBARARE  
JANUARI 2021.

### 1. UTANGULIZI

Napenda kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari Kidato cha Kwanza Januari 2021. Shule ya Sekondari Tambarare ipo Kata ya Kia Wilaya ya Hai. Muhula wa kwanza wa masomo utanza tarehe 11/01/2021. Hivyo unatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo saa 1:15 asubuhi.

### 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

#### a. Sare za shule – WAVULANA

- (i) Suruali mbili (2) upana chini inchi 16. Rangi imeambatanishwa
- (ii) Masharti meupe mawili (2) mikono mifupi.
- (iii) Sweta – rangi imeambatanishwa
- (iv) Viatu vyeusi vya kamba pea mbili (2)
- (v) Soksi nyeupe pea mbili (2)
- (vi) Nguo za michezo
- (vii) T-shirt ya Blue ya kola

#### b. Sare za shule – WASICHANA

- (i) Sketi za mshono wa rinda box mbili (2) na zifike chini ya magoti – Rangi imeambatanishwa.
- (ii) Masharti meupe mawili (2) mikono mifupi
- (iii) Sweta – rangi imeambatanishwa
- (iv) Soksi nyeupe pea mbili (2)
- (v) Nguo za michezo
- (vi) T-shirt ya Blue ya kola
- (vii) Viatu vyeusi vya kamba

*NB: Rangi ya Hijabu ni kitambaa cheupe.*

3. VIFAA VYA DARASANI

- Madaftari makubwa 10 counter book (Two Quire)
- Madaftari madogo 10
- Kalamu, penseli, rula na mkebe wa Hisabati (Mathematical set)
- Begi la kubebea madaftari na viatu
- Dictionary ndogo
- Fail moja na picha 1 passport size 4.

4. CHAKULA CHA MCHANA

- Shule inatoa huduma ya chakula cha mchana ambayo husimamiwa na kamati ya wazazi

5. UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA USAFI WA SHULE.

- Mwanafunzi ataleta mche mmoja wa mti ataupanda na kuutunza kwa muda wote atakapokuwa shuleni. Pia atapangiwa eneo la kufanya usafi. Pia eneo la kufyekea na ndoo ndogo ya lita kumi na ufagio aina ya chelewa.

6. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE


- Nakala ya sheria za shule imeambatanishwa

7. FOMU MBALIMBALI ZA KUJAZA

- (i) Medical Examination Form
- (ii) Fomu ya Maelezo binafsi ya mwanafunzi
- (iii) Nakala ya cheti cha kuzaliwa

8. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

Karibu sana Tambarare Sekondari



.....  
R. M. SWAY  
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI TAMBARARE  
S.L.P. 278 HAI

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu No 25 ya mwaka 1978.aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa nakala yake mara ya kuripoti shuleni

- a) Heshima kwa viongozi ,wazazi ,wanafunzi , wafanyakazi wote ,na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
- c) Kuwahi shuleni na kuzingatia ratiba ya shule
- d) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- e) Kuvaa sare za shule wakati wowote unapotakiwa
- f) Kufahamu mipaka ya shule

## MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHIA KUFUKUZWA SHULE

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji wa bangi ,mirungi kubeli.
- e) Kupigana na kupiga
- f) Kudharau bendera ya taifa
- g) Kuoau au kuoielewa
- h) Kupata mimba au kuharibu mimba ndani au nje ya shule
- i) Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo inayovuruga amani na usalama wa shule
- j) Kukataa adhabu kwa makusudi
- k) Kumiliki simu shuleni

SHULE YA SEKONDARI TAMBARARE  
MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi \_\_\_\_\_ (Majina 3 kwa herufi kubwa)
2. Jinsia: Mvulana / Msichana \_\_\_\_\_
3. Tarehe ya kuzaliwa \_\_\_\_\_
4. Kijiji \_\_\_\_\_ Kata \_\_\_\_\_  
Tarafa \_\_\_\_\_ Wilaya \_\_\_\_\_  
Mkoa \_\_\_\_\_
5. Dini \_\_\_\_\_ Dhehebu \_\_\_\_\_
6. Namba ya mtihani STD VII \_\_\_\_\_ Mwaka \_\_\_\_\_
7. Jina la baba/Mlezi \_\_\_\_\_  
Kazi yake \_\_\_\_\_  
Mahali anapoishi \_\_\_\_\_  
Kata \_\_\_\_\_ Tarafa \_\_\_\_\_  
Wilaya \_\_\_\_\_ Mkoa \_\_\_\_\_  
Simu \_\_\_\_\_
8. Majina mengine ya ndugu wanaohusika na malezi ya mwanafunzi (Ni hawa tu watakaoruhusiwa kuwasiliana na uongozi wa shule kwa malezi ya huyu mwanafunzi)
  - (a) Ndugu: \_\_\_\_\_  
S. L. P \_\_\_\_\_  
Simu: \_\_\_\_\_  
Kazi yake: \_\_\_\_\_
  - (b) Ndugu \_\_\_\_\_  
S. L. P \_\_\_\_\_  
Simu: \_\_\_\_\_  
Kazi yake: \_\_\_\_\_
9. Maelezo mengine yoyote ambayo yataweza kusaidia uongozi wa shule katika kumlea mwanafunzi huyu.  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

.....  
JINA NA SAINI YA MWANAFUNZI

.....  
JINA NA SAINI YA MZAZI/MLEZI

FOMU IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI  
NA KUMPA MKUU WA SHULE.

Mimi (Jina la mganga mkuu wa Mkoa / Wilaya) \_\_\_\_\_

Ninadhibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi) \_\_\_\_\_

Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/hana Afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:-

A: HALI YA MWILI

(i) Mapigo ya Moyo \_\_\_\_\_

(ii) Haemoglobini \_\_\_\_\_

(iii) Kundi la damu (Blood group) \_\_\_\_\_

(iv) Mkojo \_\_\_\_\_

(v) Kinyesi \_\_\_\_\_

(vi) Macho yana kasoro \_\_\_\_\_

(vii) Masikio yana kasoro \_\_\_\_\_

(viii) Angalia; weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (A) i-vii

B: MAGONJWA

Amewahi/hajawahi/au/hana magonjwa yafuatayo:-

(a) Bronchial Asthmas \_\_\_\_\_

(b) Tuberculosis \_\_\_\_\_

(c) Epilepsy \_\_\_\_\_

(d) Blood pressure \_\_\_\_\_

(e) Sick cells \_\_\_\_\_

(f) Peptic/D \_\_\_\_\_

(g) Ukoma \_\_\_\_\_

(h) Venereal diseases (give type) \_\_\_\_\_

(i) Mental illness (ugonjwa wa akili) \_\_\_\_\_

(j) Any other diseases not mentioned above \_\_\_\_\_

.....  
Sahihi na Mhuri wa Daktari /Mganga

Tarehe : .....

\*Futa neno lisilohusika.